



Maswali na majibu (jinsia)

Q. Ukimwi una dhuru nani wanaume ama wanawake?

Siku hizi nambari ya wanaume na wanawake wanaoishi na virusi vya ukimwi vinatoshana , lakini hapo awali nambari ya wanaume ili zidi ya wanawake .Lakini siku hizi wanawake nambari ya wanawake imeongezeka : wanawake wametoka aslimia thelathini na tano hadi asilimia arobaini na nane wanaoishi na virusi vya ukimwi na asilimia sitini ya wasichana kati ya umri wa kumi tano hadi ishirini na nne , Afrika wanawake wanaoishi na virus vya ukimwi ni asilimia hamsini na tisa.

Q. Wanawake wana hatari kubwa wakati wa kufanya mapenzi?

Ndio , wanawake wana hatari kubwa ya kupitishiwa virusi wanapofanya mapenzi na mtu mwenye virusi vya ukimwi ikilinganishwa na wanaume ambao hawana hatari kubwa ya kushikwa na virusi wanapofanya mapenzi na mtu mwenye virusi vya ukimwi.

Q. Je kuhusa jamii?

Jamii huwa haitoshanishi wanawake na wanaume na mara mingi wanaume wana weza fanya vile wanavyotaka n apia kuwa na wapenzi wengi na hii inaongeza nambari ya wanawake wenye virusi vya ukimwi . Mwana chama wa UN alisema mpaka wanawake waweze kujitetea wakati wa kufanya mapenzi na kujichunga basi wataendelea kuadhiriwa na virusi vya ukimwi.

Q. kuna mambo mengine yanayoweka wanawake kwenye hatari?

Ndio , mara kwenye nchi zinazoendelea wanawake hutaka kuongezwa damu na hii inaweza kuwa njia ya kupata virusi vya ukimwi , pia wanawake kutegemea wanaume kwa kila kitu na kwa hivyo wanawake hawatafuti kazi na wanategemea wanaume kwa kila kitu. Pia ukahaba ambapo wasichana wadogo wanatafuta wanaume wazee ili wapate pesa na vitu vizuri na virusi vinapitishwa kutoka hawa wazee mpaka kwa wasichana hawa.

Q. Wanawake ndi o watu muhimu kwenye familia ,nini hufanyika wanapokuwa wagonjwa?

Wamama ndio huchunga jamii zao , kwa kawaida mtu akiwa mgonjwa kwenye familia wanawake ndio huwachunga ,mwanaume akiwa mgonjwa haendi kazini kwahivy hakuna pesa na hii inabidi watoto wakae nyumbani , wakati mama anakuwa mgonjwa .Mara mingi watoto huwa mayatima na wanaanza kujichunga wenyewe , hivi sasa kuna mayatima milioni kumi na nne ,ili kubalisha hii ni lazima tubadilike , tubadili tabia zetu ,tujue hali zetu na kufundisha watu wengine kuhusu ugonjwa huu wa ukimwi.